www.repoa.or.tz

Toleo Na 2/2021 Machi 2021

REPOA Knowledge is Power

# Dokezo la Utafiti

## Uwezeshaji wa Wananawake Kwenye Uzalishaji, Utafutaji wa Kipato, Umiliki wa Raslimali na Uongozi Kupitia Mpango wa Kukuza Uwezo wa Kaya Maskini (PSSN)

Na: *Donald E. Mmari, na Paschal B. Mihyo*

Kitabu kinachohusu Uwezeshaji wa Wanawake Tanzania kama sehemu ya Sera za Kudumisha Ustawi wa Jamii (Empowering Women in Tanzania in the Contexts of Contemporary Social Policy) kimetolewa na REPOA kwa madhumuni ya kutoa uchambuzi wa kisera, matukio na taasisi ambazo ni sehemu ya mihimili ya jitihada za serikali za kuwawezesha wanawake Tanzania. Dokezo hili linatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti yanayoonyesha mchango wa TASAF kupitia Mpango wa Kukuza Uwezo wa Kaya Maskini katika kuwaongezea uwezo wanawake kwenye uzalishaji mali, utafutaji wa kipato, umiliki wa rasilimali na ushirikishwaji kwenye uongozi.

### MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA

- TASAF kupitia PSSN imetoa mchango mkubwa na ikiongezewa uwezo zaidi itakuwa chachu kubwa kwa maendeleo ya wanawake.
- Mipango ya TASAF inaweza kuwa na kasi kubwa zaidi ikishirikisha asasi zisizo za serikali kutoa elimu kuhusu haki na usawa wa kijinsia.
- Maeneo mengi ya kuichumi yameonyesha mafanikio makubwa kwenye kuwawezesha wanawake.
- TASAF ikipanua wigo na kuingiza makundi mengine ya watu maskini inaweza ikainua watu wengi zaidii kutoka kwenye umaskini.

### Utangulizi na Madhumuni

Tangu mwanzo wa milenia hii, Tanzania imetekeleza mipango kadhaa yenye madhumuni ya kuimarisha ustawi wa jamii iliyolenga uwezeshaji wa wanawake na makundi yenye uwezo mdogo kwenye jamii. Miongoni mwa mipango hii ni kuundwa kwa TASAF mwaka 2000 na Baraza La Taifa La Uwezeshaji Kiuchumi (NEEC) mwaka 2005. Mpango mkubwa ulioasisiwa na TASAF ni Mpango wa Kukuza Uwezo wa Kaya Maskini (PSSN) ambao huzisaidia kaya maskini sana ukizilenga kaya zenye watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, wakongwe na wanakaya wengine wenye magonjwa sugu. Kwa vile kwenye kaya nyingi zilizolengwa huduma za kijamii hutolewa na wanawake, utafiti ulijikita kwenye kuchunguza ni kwa kiwango gani fedha na misaada inayotolewa na TASAF kupitia mpango wa PSSN imechangia kwenye uwezeshaji wa wanawake kwa kuwaongezea uwezo kiuchumi, kisiasa na kwenye kuboresha mchango wao kwenye maendeleo yao, ya kaya zao na ya jamii. Kitabu hiki kilitokana na Programu ya utafiti wa REPOA kuhusu Maendeleo na Fursa za Kiuchumi kwa Wanawake (Growth and Economic Opportunities for Women – kifupi

GrOW) uliofadhiliwa na shirika la maendeleo ya utafiti, yaani International Development Research Centre (IDRC) la Canada kwa ushirika na William and Flora Hewlett Foundation ya Marekani na iliyokua Idara ya Maendeleo ya Kimataifa, yaani Department for International Development (DFID) ya Uingereza. Madhumuni ya utafiti yalikuwa ni kupima kiwango cha uwezeshaji wa wanawake utokanao na mpango wa TASAF wa kujenga uwezo wa kaya maskini na kuangalia kama fedha yenye masharti zinayotolewa kwa walengwa zina mchango wa moja kwa moja kwenye uwezeshaji wa wanawake.

## Mbinu za utafiti zilizotumiwa

Utafiti ulikuwa shirikishi na ulikuwa na awamu mbili: utafiti wa awali na utafiti raundi ya pili. Watafiti walishirikiana kwa karibu sana na kamati za serikali ngazi za vijijini, halmashauri, mkoa na taifa and pia asasi za kiaraia zilihusishwa. Watafiti walitumia viashiria vitano vilivyotolewa kwenye kielezo kiitwacho 'Women Empowerment in Agriculture Index (WEAI)' kinachotumiwa kupima uwezeshaji wa wanawake kwenye sehemu tano: uzalishaji, rasilimali za uzalishaji, kipato, uongozi na matumizi ya muda wao.[1] Utafiti ulitumia takwimu na taarifa za wingi na ubora wa matokeo baada ya kuwahoji walengwa kwenye jumla ya kaya 1,935, wakiwemo zaidi ya wanaume na wanawake 11,000 wenye umri wa miaka 18 au zaidi kwenye wilaya 9 zilikoanzia shughuli awamu za awali za TASAF (Maarufu kama TASAF's Program Authority Areas-PAA) kwa kipindi cha miezi 36 tangu Novemba 2014. Jumla ya vijiji 102 kwenye wilaya 11 vilifanyiwa utafiti zikiwemo kaya 15 hadi 18 kila kijiji zilizochaguliwa kwa nasibu yaani bila kutumia vigezo maalum. Wilaya zilizohusika Tanzania Bara ni Misungwi, Kahama, Kilosa, Kisarawe, Handeni, Mbogwe, Itilima and Uyui. Kwa upande wa Zanzibar, wilaya moja ilichaguliwa. Wilaya za Bagamoyo and Chamwino za Tanzania Bara ambazo ziliishafanyiwa utafiti na TASAF awali, ziliongezwa kwenye idadi.

[1] IFPRI, 2012 Women Empowerment in Agriculture Index

## Matokeo ya Utafiti

### Ushirikishwaji wa Wanawake kwenye uzalishaji

Uchambuzi wa takwimu na taarifa zilizotokana na utafiti wa awali wa mwaka 2014 unaonyesha kwamba wanaume walikuwa na uwezo zaidi ya wanawake; tofauti kwenye uwezo kati ya wanawake na wanaume kwa ujumla ulikuwa ndogo; lakini tofauti hizo hazikulingana kwenye kila eneo. Hata hivyo uchambuzi wa matokeo ya utafiti wa awali na ule wa raundi ya pili wa mwaka 2017 kwa pamoja yanonyesha kwamba TASAF kupitia PSSN imewawezesha wanawake. Pia uchambuzi wa uwezeshaji wa wanawake kwenye maeneo tisa ulionyesha kwamba uwezo wao ulikuwa bado chini ya ule wa wanaume kwenye maeneo saba ingawaje kwenye masuala yanayohusu matengenezo ya nyumba, uwezo wa jinsia zote mbili unakaribiana sana na ushiriki wa wanawake kwenye shughuli za kaya ni mkubwa zaidi ya ule wa wanaume. Utafiti unaonyesha pia kwamba ukilinganisha matokeo ya utafiti wa awali na ule uliofuatia, vitu vitatu vinajitokeza. Kwanza kwenye maeneo ya uvuvi, kilimo cha mazao ya biashara ushiriki wa wanawake kwenye matokeo ya awali ulikuwa chini na kwenye matokeo ya utafiti wa pili uliendelea kushuka. Pili, kuhusu kilimo cha mazao ya chakula, takwimu za ushiriki hazikuwa na mabadiliko yoyote. Tatu, kwenye maeneo ya ufugaji, kazi za kuajiriwa, shughuli zisizo za kilimo, akiba ya fedha na matengenezo ya nyumba, ushiriki wa wanawake uliongezeka kwa kiasi kikubwa na kuzidi ule wa wanaume. Kwa undani anagalia Jedwali Namba 1.

**Jedwali Namba 1: Ushiriki katika uzalishaji na utafutaji wa kipato**

| Shughuli | Matokeo ya awali | Matokeo yaliyofuata | Badi-liko(%) |
|---|---|---|---|
| Kilimo cha mazao ya chakula | 96.44 | 94.17 | -2.27 |
| Kilimo cha mazao ya biashara | 84.0 | 68.74 | -15.26 |
| Ufugaji | 95.8 | 100.99 | 5.19 |
| Ajira na ujira | 95.8 | 165.70 | 69.9 |
| Shughuli zisizo za kilimo | 98.6 | 156.77 | 58.17 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Shughuli za TASAF za kujikimu au PWP | 107 | 143.74 | 36.74 |
| Uvuvi na ufugaji samaki | 78 | 49.40 | -28.6 |
| Akiba ya fedha | 95.08 | 193.91 | 98.83 |
| Matengenezo ya nyumba | 100 | 158.26 | 58.26 |
| Wastani | | | 31.21 |

## Ushiriki wa wanawake kwenye maamuzi kuhusu matumizi

Kwenye awamu zote za utafiti wahojiwa waliulizwa kiasi cha mchango wao kwenye maamuzi yaliyohusu maeneo tisa. Uchambuzi wa takwimu unaonyesha wanaume walikuwa na mchango mkubwa kuliko wanawake. Kwenye maswali ya mifugo na akiba mchango wa wanawake na wanaume ulikuwa karibu sawa lakini kwenye shughuli zitokanazo na PSSN mchango wa wanawake ulikuwa zaidi ya ule wa wanaume.

## Mchango wa wanawake kwenye maamuzi kuhusu kipato

Takwimu zilizotokana na utafiti wa awali zinaonyesha kwamba kwa wastani, wanaume walikuwa na mchango mkubwa kuliko wanawake kuhusu njia za kutengeneza mapato lakini utafiti uliofuatia wa baadaye ulionyesha kwamba wanawake walikuwa na mchango zaidi kwenye maamuzi kuhusu matumizi ya mapato yatokanayo na mpango wa PSSN. Hata hivyo, mchango wao ulikuwa karibu sawa na ule wa wanaume kwenye maamuzi yaliyohusu mapato yaliyotokana na ufugaji na uwekaji wa akiba. Mchango wao ulikuwa mdogo kwenye maamuzi kuhusu kipato kilichotokana na shughuli nyinginezo.

**Jedwali Namba 2: Mchango kwenye maamuzi kuhusu kipato**

| Shughuli | Matokeo ya awali | Matokeo yaliyofuata | Badiliko |
|---|---|---|---|
| Kilimo cha mazao ya chakula | 3.46 | 3.76 | .30 |
| Kilimo cha mazao ya biashara | 3.31 | 3.46 | .15 |
| Ufugaji | 3.43 | 3.72 | .29 |
| Shughuli zisizo za kilimo | 3.73 | 3.99 | .26 |
| Ajira na ujira | 3.55 | 3.72 | .17 |
| Shughuli za TASAF za kujikimu au PWP | 3.57 | 4.06 | .49 |
| UVuvi na ufugaji wa samaki | 2.17 | 3.06 | .89 |
| Akiba ya fedha | 3.69 | 3.74 | .05 |
| Matengenezo ya Nyumba | **2.84** | **3.06** | **.22** |

## Ushiriki wa wanawake kwenye maamuzi kuhusu umiliki wa raslimali

Uchambuzi wa takwimu zilizotokana na utafiti wa awali na ule uliofuatia unaonyesha kwamba wanawake wamewezeshwa zaidi kwenye maamuzi yanayohusu kilimo cha mazao ya chakula, ufugaji na shughuli zisizo za kilimo pamoja na uwekaji wa akiba ya fedha. Kiwango cha uwezeshwaji kilikuwa juu zaidi kwenye maeneo ya ajira na ujira, matengenezo ya nyumba na haki ya kumiliki rasilimali kama inavyoonyeshwa kwenye Jedali Namba 3.

**Jedwali Namba 3: Haki ya matumizi ya matokeo ya shguli mbali mbali**

| Shughuli | Matokeo ya awali | Matokeo yaliyofuata | Badiliko |
|---|---|---|---|
| Kilimo cha mazao ya chakula | 2.86 | 3.0 | .14 |
| Kilmo cha mazao ya biashara | 2.79 | 2.94 | .15 |
| Ufugaji | 2.91 | 3.01 | .10 |
| Shughuli zisizo za kilimo | 3.07 | 3.21 | .14 |
| Ajira na ujira | 2.74 | 3.05 | .31 |
| Shughuli za TASAF za kujikimu au PWP | 2.71 | 2.23 | -.48 |
| Uvuvi na ufugaji wa samaki | 1.81 | 3.35 | 1.54 |
| Akba ya fedha | 3.09 | 3.22 | .13 |
| Matengenezo ya nyumba | 2.41 | 2.82 | .41 |

## Ushiriki wa Wanawake kwenye uongozi

Uchambuzi unaonyesha kwamba ingawaje tofauti ya kijinsia inazidi kupungua kwenye shuguli za ndani ya kaya, tofauti ni kubwa kwenye eneo la uongozi hasa kuhusu ushiriki kwenye vikundi na kuongea kwenye vikao au hadharani kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Namba 4. Tafsiri yake ni kwamba ingawa misaada yenye masharti inayotolewa na TASAF ni wezeshi kwa wanawake ndani ya kaya zao, bado wanahitaji misaada ya aina nyingine ambao inaweza kuwaongezea sauti nje ya kaya zao.

**Jedwali Namba 4: Mawazo ya wahojiwa kuhusu kiwango chao cha kuchagia maswali ya maendelo kwenye vikao**

| Suala | Utafiti wa awali | Utafiti uliofuata | Badiliko |
|---|---|---|---|
| Miundombinu | 2.1 | 2.12 | +.02 |
| Ujira sahihi kwenye Miradi ya kujikimu | 2.01 | 2.07 | +.06 |
| Maadili ya viongozi | 2.01 | 2.12 | +.11 |
| Maendeleo ya jamii | 2.15 | 2.16 | +.01 |
| Kamati za msingi | 2.04 | 2.17 | +.13 |
| Manbo yanayohusu kaya | 3.93 | 3.73 | -.20 |
| Mambo ya ndoa | 3.98 | 3.8 | -.18 |

## Hitimisho

Inaelekea kwa ujumla kwamba wanaume wana uwezo zaidi kuliko wanawake lakini pia ni wazi kwamba kwenye miradi ya PSSN wanawake wamewezeshwa. Pili ni dhahiri kwamba uwezeshaji uliojitokeza kwenye shughuli za PSSN hauna uhakika wa kuwa endelevu mpango huu utakapomalika. Tatu, ili uwezeshaji wa wanawake uwe endelevu, kunahitajika mbinu mpya zitakazoingiza mafunzo ya stadi na ujasiriamali kwa walengwa ili kuwaongezea uwezo wa kujipatia kipato na kujitegemea. Nne, uwezeshaji kupitia maendelo ya wanawake utafanikiwa zaidi ukiambatana na elimu ya uongozi na ushirkiswaji kwenye maamuzi kwenye jamii.

## Mapendekezo

**Kutokana na utafiti huu inapedekezwa kwa TASAF:**

- *Kufanya tathmnini* yakinifu ya maeneo ambako uwezeshaji umedhihirika, kwa mfano kazi za ajira na nyinginezo zinazoambatana na ujira na kuyaongezea nguvu kifedha.
- *Kupima ramani mpya ya umaskini* ili kubani kaya zinazotishiwa kuingia kwenye dhiki au umaskini wa kupokezana toka kizazi hadi kizazi, ili kuhakikisha hakuna aliyeachwa nyuma.
- *Kuongeza misaada kwenye maeneo yanayowaongezea* wanawake uwezo wa kujieleza na kushiriki kwenye maamuzi kwenye jamii ili ongezeko la sauti yao liwasaidie kujionegezea uwezo kiuchumi na haki za miliki.
- *Kutafuta njia za kupanua wigo* ili kuwaingiza kwenye mfumo wajane, wanaume wenye majukumu ya kutunza kaya zisizojiweza na wale ambao wamekumbwa na umaskini wakurithi.
- *Kuingiza kwa uwazi zaidi maswali ya usawa wa jinsia kwenye miradi ya PSSN* na kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali katika kuwaelimisha walengwa kuhusu haki na usawa wa kijinsia.

REPOA
157 Mgombani/REPOA Street, Regent Estate
P.O. Box 33223, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2700083, Cell: +255 75 409 1677 Fax +255 22 2705738
Website: www.repoa.or.tz Email:repoa@repoa.or.tz

Kituo cha Taarifa na Maarifa, REPOA
Kituo chetu cha Taarifa na Maarifa kinatoa mazingira mazuri kwa utafiti wa fasihi na vitabu/ maandiko mbali mbali kwa haraka na kwa urahisi wa matumizi ya maarifa na taarifa. Imeunganishwa na wavuti (internet) kwa ajili ya matumizi ya maktaba ya mkondoni (online) kuwasaidia wanaosomea Shahada za Uzamili na Uzamivu, watafiti na wasomi kwa kuwapatia magazeti, vitabu, ripoti n.k. ya siku za karibuni.

Saa za Ufunguzi
Kituo cha Taarifa na Maarifa kinakuwa wazi kuanzia Jumanne hadi Ijumaa saa 4.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana, saa 8.00 mchana hadi saa 11.00 alasiri. Maktaba ya mkondoni (online) ni wazi saa 24 kila siku.

@REPOA 2021
Matokeo, tafsiri, hitimisho, na maoni yaliyotolewa humu ndani ni ya mwandishi na siyo lazima yawe yanaakisi maoni na sera za REPOA.